JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

TUME YA TAIFA YA MIPANGO YA MATUMIZI YA ARDHI

# MKAKATI WA KUKABILIANA NA CHANGAMOTO ZA MATUMIZI BORA YA ARDHI NCHINI

OKTOBA 2017

## YALIYOMO

1. Utangulizi........................................3

2. Chimbuko la Mkakati........................................4

3. Malengo ya Mkakati........................................5

4. Changamoto na Mapendekezo Kuhusu Upangaji, Utekelezaji na Usimamizi wa Mipango ya Matumizi ya Ardhi Nchini........................................8

5. Mkakati wa Kutatua Changamoto za Upangaji, Utekelezaji na Usimamizi wa Mipango ya Matumizi ya Ardhi........................................13

5.1 Mpango Kazi wa Kupatia Suluhisho Changamoto na Kutekeleza Mapendekezo Yaliyotolewa na Wadau........................................14

5.2 Mpango wa Elimu kwa Umma Juu ya Masuala Mbalimbali Yanayokabili Upangaji, Utekelezaji na Usimamizi wa Matumizi ya Ardhi Nchini........................................24

# 1. UTANGULIZI

Ardhi ni rasilimali ya msingi katika kuleta maisha bora kwa kila Mtanzania kwani ni muhimili wa maisha ya wananchi walio wengi hususan waishio vijijini. Ardhi ikipangwa, kupimwa, kumilikishwa na kutumika ipasavyo ni muhimu kwa maendeleo ya kiuchumi, kuwepo kwa usalama wa chakula na mtaji muhimu katika kuondoa umasikini. Hivyo, tija itokanayo na rasilimali ardhi inaweza kuongezwa kwa kuandaa na kutekeleza mipango ya matumizi ya ardhi.

Mipango ya matumizi ya ardhi huwezesha jamii kufanya maamuzi na kutafsiri malengo mahususi ili kupata maendelo endelevu. Misingi muhimu katika hili ni (a) Kuimarisha taasisi na mbinu za uratibu (b) Kuboresha na kuimarisha mifumo ya usimamizi wa mipango ya matumizi ya ardhi na (c) Kuweka utaratibu ili kuwezesha ushirikishwaji na ushiriki wa wananchi katika ngazi mbali mbali. Upangaji wa matumizi ya ardhi unatoa mwongozo wa jumla wa usimamizi wa rasilimali ardhi na kuweka uhusiano mpana baina ya mifumo ya asili, ya kijamii na kiuchumi katika uzalishaji. Upangaji wa matumizi ya ardhi kwa ushirikishwaji unazingatia uchambuzi, majadiliano na utoaji wa maamuzi katika jamii na sekta mbalimbali.

Moja ya malengo ya jumla ya upangaji wa matumizi ya ardhi ni kuhahikisha kunakuwepo na matumizi bora ya rasilimali za ardhi ambazo haziongezeki. Hili linaweza kufanikiwa kwa kuwepo kwa taasisi zilizo imara na njia madhubuti za uratibu ambazo zitajenga utaratibu wa mawasiliano yatakayowezesha uhusishwaji na ushiriki wa wananchi katika ngazi za chini. Uratibu miongoni mwa sekta zinazohusiana na masuala ya ardhi ni muhimu kutokana na kuongezeka kwa mahitaji ya kusimamia matumizi ya rasilimali ardhi na kuongezeka kwa ufahamu kwamba matatizo ya usimamizi wa matumizi ya ardhi hupatiwa ufumbuzi kwa njia ya ushirikishwaji.

Pia, ili kuimarisha ushirikiano baina ya Serikali Kuu, Serikali za Mitaa, Taasisi za Serikali, Asasi za Kiraia na Wadau wengine wanaojihusisha na upangaji wa matumizi ya ardhi nchini, Sheria ya Upangaji Matumizi ya Ardhi Namba 6 ya Mwaka 2007

inatambua dhana ya ushirikishwaji katika upangaji, upimaji, umilikishwaji na usimamizi wa matumizi ya ardhi kwa kuunda Mamlaka za Upangaji katika ngazi ya Taifa, Wilaya, Vijiji na mamlaka yoyote itakayoteuliwa na Waziri kuwa mamlaka ya upangaji. Hata hivyo, kutokuwepo kwa uratibu wa kutosha baina ya sekta zinazohusiana na ardhi katika kusimamia kazi za upangaji wa matumizi ya ardhi; uelewa mdogo wa wananchi na kutofahamu sheria za ardhi, na miongozo ya upangaji matumizi ya ardhi kama vile Sheria ya Ardhi Namba 4 ya Mwaka 1999, Sheria ya Ardhi ya Vijiji Namba 5 ya Mwaka 1999, Sheria ya Utatuzi wa Migogoro ya Ardhi Namba 2 ya Mwaka 2002 na Sheria ya Upangaji wa Matumizi ya Ardhi Namba 6 ya Mwaka 2007 kulichangia kuwepo kwa hitaji la kufanyika kwa mkutano wa wadau ili kujadili changamoto hizi na kuzipatia ufumbuzi wa kudumu.

## 2. CHIMBUKO LA MKAKATI

Chimbuko la Mkakati huu ni utekelezaji wa sheria za Ardhi ambazo zimetokana na Sera ya Taifa ya Ardhi ya mwaka 1995. Sera hii imeweka misingi ya upangaji, utekelezaji na usimamizi wa matumizi ya ardhi wenye lengo la kuimarisha miliki za ardhi, kuwezesha matumizi endelevu ya rasimali zilizo juu ya ardhi kwa ajili ya maendeleo ya kiuchumi na kijamii.

Sera zingine ambazo zinatoa misingi ya usimamizi endelevu wa rasilimali ardhi na mazingira ni pamoja na Sera ya Taifa ya Mazingira ya Mwaka 1997 na Sera ya Maendeleo ya Makazi ya Mwaka 2000. Vilevile, Sera ya Madini, Sera ya Wanyamapori, Sera ya Uvivu, Sera ya Kilimo na Sera ya Nishati zimefanyiwa marekebisho ili kuongeza msisitizo kuhusu ardhi na usimamizi wa mazingira, kupata ufumbuzi wa tatizo la uhamiaji mijini na kuongeza tija katika kilimo, ufugaji na uwekezaji

Kutokana na kuwepo kwa changamoto mbalimbali ambazo zinakwamisha kuwepo kwa ufanisi katika kupanga, kutekeleza na kusimamia mipango ya matumizi ya ardhi nchini, Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi kwa Kushirikiana na Asasi za Kiraia za Care International-Tanzania, Jumuiko la Maliasili Tanzania na Oxfam Tanzania iliandaa Mkutano wa wadau ili kujadili changamoto, kubadilishana uzoefu,

kutambua fursa na kupata mapendekezo ya kuongeza ufanisi katika upangaji, utekelezaji na usimamizi wa mipango ya matumizi ya ardhi. Mkutano huo ulifanyika tarehe 04-05 Agosti 2016 na kuhudhuriwa na wadau mbalimbali kutoka Wizara na Taasisi za Serikali, Mashirika Binafsi, Asasi za Kiraia na baadhi ya Washirika wa Maendeleo. Kutokana na Mkutano huo, wadau walipendekeza kuandaliwa kwa mkakati wa utekelezaji wenye lengo la kukabiliana na changamoto mbalimbali za upangaji, utekelezaji na usimamizi wa mipango ya matumizi ya ardhi nchini.

## 3. MALENGO YA MKAKATI

### 3.1 LENGO KUU LA MKAKATI

Lengo kuu la mkakati huu ni kuainisha mikakati ya kukabiliana na changamoto za upangaji, utekelezaji na usimamizi wa mipango ya matumizi ya ardhi nchini

### 3.2 MALENGO MAHSUSI YA MKAKATI

Malengo mahsusi ya Mkakati ni kama ifuatavyo;

#### 3.2.1 Kuimarisha Uratibu na ushirikiano wa Wadau katika upangaji, utekelezaji na usimamizi wa mipango ya matumizi ya ardhi

Moja ya malengo ya jumla ya upangaji wa matumizi ya ardhi ni kuhahikisha kunakuwepo na matumizi bora ya rasilimali za ardhi ambazo haziongezeki. Uratibu miongoni mwa sekta zinazohusiana na masuala ya ardhi ni muhimu kutokana na kuongezeka kwa mahitaji ya kusimamia matumizi ya rasilimali ardhi na kuongezeka kwa ufahamu kwamba matatizo ya usimamizi wa matumizi ya ardhi hupatiwa ufumbuzi kwa njia ya ushirikishwaji. Uratibu wa wadau utahusisha ujengewaji wa uwezo wadau (mamlaka zote za upangaji) katika maeneo mbalimbali nchini juu ya miongozo ya upangaji, utekelezaji na usimamizi wa matumizi ya ardhi

Wadau wa mipango ya matumizi ya ardhi wataongozwa na Mpango wa Taifa na mikakati yake katika kupanga, kutekeleza na kusimamia matumizi ya ardhi nchini.

### 3.2.2 Kuwezesha uandaaji wa mipango ya matumizi ya Ardhi ya Wilaya 25 na Vijiji 7500 hadi kufikia mwaka 2020

Mkakati umelenga kuhakikisha kuwa mipango ya matumizi ya ardhi ya Wilaya 25 na Vijiji 7,500 inakamilishwa hadi kufikia mwaka 2020. Kutokana na kuwepo na kasi ndogo ya upangaji matumizi ya ardhi nchini inayosababishwa na uwepo wa rasilimali chache, Mkakati huu umelenga kuwashirikisha wadau wote nchini wanaojihushisha na upangaji wa matumizi ya ardhi ili waweze kupanga kwa pamoja na kuwa na malengo ya pamoja katika upangaji, utekelezaji na usimamizi wa mipango ya matumizi ya ardhi. Kupitia utambuzi wa wadau uliofanyika na unaoendelea kufanyika, malengo ya wadau kitaasisi, maeneo wanayofanyia kazi na fursa walizo nazo umefanyika ili kujua mtawanyiko wa upangaji wa matumizi ya ardhi nchini. Uchambuzi huu utasaidia katika kuweka mfumo wa kuelekeza rasilimali kwenye maeneo mbalimbali nchini baina ya wadau wote.

Kupitia uratibu wa wadau, Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi itaweza kupata takwimu za mipango inayoandaliwa kote nchini na pia kushirikisha wadau ili kujumuisha rasilimali walizo nazo ili waweze kupanga matumizi ya ardhi ya vijiji vingi kwa wakati mmoja. Vile vile utekelezaji wa Mkakati huu utachangia juhudi za Serikali kuhakikisha kuwa Mpango wa Taifa wa Matumizi ya Ardhi 2013 – 2033 unazingatiwa na kutekelezwa na wadau wote nchini.

### 3.2.3 Kukabiliana na Migogoro ya Matumizi ya Ardhi baina ya Watumiaji Mbalimbali

Migogoro ya matumizi ya ardhi imeendelea kuongezeka katika maeneo mbalimbali hapa nchini. Upangaji, utekelezaji, usimamizi na ufuatiliaji wa mipango ya matumizi ya ardhi utasaidia kuondoa migogoro ya matumizi ya ardhi. Kupitia Mkakati huu, mpango wa elimu kwa umma umeandaliwa ambao malengo yake ni kuhakikisha kuwa wadau wote hasa wananchi wanapata uelewa wa umuhimu wa mipango ya matumizi ya ardhi zikiwemo Sheria zinazosimamia rasilimali za ardhi (mfano Sheria za Ardhi, Mazingira, Kilimo, Mifugo, Misitu, Maji na Madini). Ili kupata suluhisho la

kudumu la migogoro ya ardhi, Mkakati umelenga kuzihamasiha Taasisi zote za elimu, dini na jamii katika ngazi zote na kuhakikisha kuwa masuala ya upangaji, utekelezaji, usimamizi na usuluhishi wa migogoro ya ardhi inaingizwa katika Mitaala ya kufundishia ili kuwepo na kizazi chenye ufahamu na umuhimu wa kulinda na kuheshimu rasilimali ardhi nchini na hivyo kuondokana na migogoro ya matumizi ya ardhi

### 3.2.4 Kuwezesha Upatikanaji wa Ardhi kwa Ajili ya Uwekezaji Mbalimbali

Kuandaliwa kwa mipango mingi ya matumizi ya ardhi nchini kutawezesha upatikanaji wa ardhi kwa ajili uwekezaji mbalimbali hasa katika sekta ya Kilimo na Viwanda. Kupangwa na kutekelezwa kwa mipango ya matumizi ya ardhi kutawezesha matumizi ya ardhi isiyokuwa na migororo kwa ajili ya uwekezaji na hivyo kuimarika kwa sekta ya viwanda. Vile vile, utekelezaji wa mipango ya matumizi ya ardhi utaweka usawa wa mahitaji ya uwekezaji na umiliki wa ardhi kwa watumiaji na wawekezaji na hivyo kuwepo na usalama wa milki kwa wahusika wote (Wamiliki wa Ardhi).

### 3.2.5 Kuwawezesha Wananchi Kiuchumi kwa Kutumia Ardhi

Kupitia utekelezaji wa mipango ya matumizi ya ardhi, wananchi huelimishwa juu ya njia mbadala za kujiongezea kipato kwa kutambua na kutumia fursa zilizopo katika maeneo yao (*Physical, natural, institutional, social and human assets).* Utambuzi wa fursa hizi na mipango kazi ya utekelezaji inazingatia upatikanaji wa ajira mpya za kujiongezea kipato kwa wananchi wa maeneo mbalimbali. Vile vile, utoaji wa hati miliki za kimila husaidia kuweka usalama wa milki wa wananchi na pia hati hizi huweza kutumiwa katika mipango ya kibiashara kwa ajili ya dhamana ya mikopo. Ushiriki wa Asasi za Kiraia katika utekelezaji Mkakati huu utawezesha kufanikiwa kwa lengo hili kwani Asasi hizi hujishughulisha na masuala mbalimbali yanayohusiana na ardhi katika kupunguza umaskini wa wananchi katika maeneo wanayofanyia kazi. Hivyo Mkakati huu umelenga katika kupunguza umaskini kwa wananchi kwa kubainisha fursa za kujiongezea kipato.

### 3.2.6 Kuweka Mfumo wa Kuwezesha Upatikanaji wa Rasilimali kwa ajili ya Kupanga, Kutekeleza na Kusimamia Mipango ya Matumizi ya Ardhi

Kwa sasa, gharama ya upangaji matumizi ya ardhi kwa kijiji kimoja (hatua ya 1 -4) ni kati ya Shilingi Milioni 15 hadi 18 kutegemeana na jiografia ya kijiji na uwepo wa migogoro ya ardhi (mipaka na matumizi). Gharama hii kwa kijiji kimoja hupungua endapo vijiji vingi katika Wilaya moja vitapangiwa matumizi ya ardhi kwa wakati mmoja.

Vilevile, kutokana na uhaba wa fedha kwa ajili ya kuwezesha upangaji, utekelezaji na usimamizi wa mioango ya matumizi ya ardhi nchini, Mkakati huu umeweka utaratibu wa uratibun na ushirikiano kifedha na kiutaalamu baina ya wadau mbalimbali katika kutekekeza Mpango Kazi wa pamoja. Vile vile, kuanzishwa kwa Mfuko wa Taifa wa Upangaji Matumizi ya Ardhi Nchini kutasaidia kuwepo kwa fedha kwa ajili ya kupanga na kutekeleza mipango ya matumizi ya arhdi nchini. Mfuko huu utapata fedha kutoka Serikalini, Mikutano ya uchangiaji (*fund raising events*) michango kutoka wadau wa matumizi ya ardhi (kama vile Asasi za Kiraia, wakulima, wafugaji n.k) na kutoka Wabia wa Maendeleo (*Development Partners).*

### 3.2.7 Kuhamasisha Uzingatiaji wa Masuala Mtambuka katika Upangaji, Utekelezaji na Usimamizi wa Mipango ya Matumizi ya Ardhi

Utekelezaji wa Mkakati huu utawezesha ushirikishwaji wa wanawake na makundi maalum katika jamii kwa lengo la kuwezesha na kuimarisha usalama wa milki. Kupitia utekelezaji wa mipango ya matumizi ya ardhi, uandaaji wa mipango kina ya matumizi ya ardhi utasaidia kwa kiasi kikubwa udhibiti wa athari zitokanazo na mabadiliko ya tabia nchi na hivyo kusaidia kuhifadhi mazingira ya vyanzo vya maji na misitu.

## 4. CHANGAMOTO NA MAPENDEKEZO KUHUSU UPANGAJI, UTEKELEZAJI NA USIMAMIZI WA MIPANGO YA MATUMIZI YA ARDHI NCHINI

Upangaji wa matumizi ya ardhi nchini huongozwa na miongozo mbalimbali ambayo inatolewa na Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi. Miongozo hiyo ni kama

vile Mpango wa Taifa wa Matumizi ya Ardhi 2013-2033, Mwongozo wa Upangaji wa Matumizi ya Ardhi ya Wilaya wa Mwaka 2006, Mwongozo wa Upangaji wa Matumizi ya Ardhi ya Vijiji wa Toleo la 2 la Mwaka 2013 na Kiongozi cha Mwanakijiji Toleo 4 la Mwaka 2013.

Pamoja na kuwepo miongozo hii, upangaji, utekelezaji na usimamizi wa mipango ya matumizi ya ardhi nchini unakumbana na changamoto mbalimbali zinazokwamisha kuwepo kwa mipango iliyo na tija kwa jamii na Taifa kwa ujumla. Kupitia Mkutano wa wadau wa Mwezi Agosti 2016, wadau wa upangaji, utekelezaji na usimamizi wa mipango ya matumizi ya ardhi waliainisha changamoto na mapendekezo mbalimbali kuhusiana na upangaji, utekelezaji na usimamizi wa matumizi ya ardhi nchini.

Baadhi ya mapendekezo yalilenga kuimarisha uratibu na ushirikiano baina ya sekta mbalimbali na kutambua dhana nzima ya upangaji wa matumizi ya ardhi kama njia muhimu kupata suluhisho la migogoro ya ardhi na uwekezaji endelevu katika ardhi.

Changamoto na mapendekezo yaliyotolewa na wadau yameonyeshwa katika **Jedwali Na. 1.** hapa chini

**Jedwali Na. 1: Changamoto na Mapendekezo ya Wadau Katika Uandaaji, Utekelezaji na Usimamizi wa Mipango ya Matumizi ya Ardhi**

| Na. | Changamoto | Mapendekezo |
|---|---|---|
| 1. | Kukinzana kwa sheria mbalimbali kunasababisha kugawanywa kwa vijiji vilivyoandaliwa mipango ya matumizi ya ardhi na kuanzishwa kwa vijiji vipya katika maeneo yaliyohifadhiwa | • Kuwepo na uratibu shirikishi ngazi zote kati ya TAMISEMI na sekta zingine kuangalia ulazima wa kugawa na kuanzisha vijiji vipya.<br>• Kabla ya kugawa vijiji, lazima kijiji kipimwe mipaka na kipangiwe matumizi ya ardhi<br>• Vijiji vyenye mipango ya matumizi ya ardhi visigawanywe hadi baada ya miaka 10 baada ya kuandaliwa mpango |
| 2. | Kutokuwepo kwa uratibu wa | Tume irejee na kuiunda upya kamati ya Uratibu |

| | | |
|---|---|---|
| | kutosha baina ya serikali, asasi za kiraia na wadau wa maendeleo katika upangaji, usimamizi na utekelezaji wa mipango ya matumizi ya ardhi. | ya Kisekta ya matumizi ya ardhi kwa kushirikisha Asasi za Kiraia na Mashirika Binafsi Uazishwe utaratibu wa kubainisha na kujumuisha kwa pamoja rasilimali fedha, utaalam na vitendea kazi kutoka kwa wadau kwa ajili ya kuandaa, kutekeleza na kusimamia mipango ya matumizi ya ardhi nchini |
| | | Uandaliwe mpango wa kutoa mafunzo kwa wakufunzi juu ya mipango ya matumizi ya ardhi ili kuwe na utaratibu mmoja wa kuandaa, kutekeleza na kusimamia mipango ya matumizi ya ardhi pamoja na kuhakikisha makundi yote ya jamii yanashirikishwa ipasavyo katika maamuzi. |
| 3. | Ufuatiliaji na tathmini hafifu ya utekelezaji wa mipango ya matumizi ya ardhi | Kuweka mfumo wa pamoja wa wadau ili kufanya tathmini na ufuatiliaji wa utekelezaji wa mipango ya matumizi ya ardhi |
| 4. | Ushiriki mdogo wa wanawake na baadhi ya makundi katika jamii kama vile wafugaji na wawindaji katika masuala ya upangaji, utekelezaji na usimamizi wa matumizi ya ardhi kutokana na mila na desturi zilizopo katika baadhi ya jamii. | Kuhakikisha na kutoa kipaumbele kwa wanawake na makundi mengine yenye ushiriki mdogo katika upangaji, utekelezaji na usimamizi wa mipango ya matumizi ya ardhi |
| 5. | Halmashauri za Wilaya kutumia muda mrefu kupitisha sheria ndogo za usimamizi wa mipango ya matumizi ya ardhi ya vijiji. | • Mwongozo wa upangaji matumizi ya ardhi ubainishe muda wa kupitisha sheria ndogo ngazi ya wilaya usiozidi mwezi mmoja baada ya kupitishwa na mkutano wa kijiji<br>• Kitengo cha Sheria kihusishwe katika hatua za upangaji ili aelewe utaratibu uliotumika na maudhui ya sheria ndogo |

| | | |
|---|---|---|
| | | zitakazotungwa pamoja na mpango wa matumizi ya ardhi kwa ujumla. |
| 6. | Katika uandaaji wa mipango ya matumizi ya ardhi ni vigumu kupata eneo la malisho linalojitosheleza katika kijiji kimoja | Wadau waandae mipango ya matumizi ya ardhi ya pamoja pale inapohitajika kufanya hivyo (joint land use plans) |
| 7. | Upangaji wa matumizi ya ardhi nchini kutopewa kipaumbele katika mipango ya kitaifa na ngazi ya halmashauri. | • Upangaji, utekelezaji na usimamizi wa mipango ya matumizi ya ardhi liwe suala la kitaifa na lipewe kipaumbele<br>• Vyombo vya habari vitumike katika kuhamasisha wadau wote (wahisani wa manedeleo na asasi za kiraia) kuongeza bajeti ya upangaji, upimaji, utekelezaji, usimamizi na ufuatiliaji wa mipango ya matumizi ya ardhi.<br>• Tume iandae mkakati wa uhamasishaji kwa viongozi na Watendaji Wakuu wa Mikoa na Halmashauri za Wilaya. |
| 8. | Halmashauri za Wilaya kama mamlaka za upangaji kutotenga bajeti za kupanga matumizi ya ardhi | OR-TAMISEMI izielekeze Halmashauri za Wilaya kutenga bajeti kwa ajili ya kuandaa, kutekeleza na kusimamia mipango ya matumizi ya ardhi |
| 9. | Kuongezeka kwa migogoro ya ardhi baina ya watumiaji mbalimbali inayotokana na kutokuwepo kwa mipango ya matumizi ya ardhi na kuhama hama kwa wakulima na wafugaji | • Mipango ya matumizi ya ardhi iandaliwe ili kutenga maeneo kwa ajili ya malisho pamoja na matumizi mengine na kuweka miundombinu muhimu mfano malambo, njia za mifugo, majosho nk.<br>• Utafiti wa kina ufanyike kutambua mfumo mzima wa maisha ya kuhama hama baina ya wakulima na wafugaji na kuangalia namna/jinsi bora ya kuuboresha mfumo huo ili kuchochea kasi ya ukuaji uchumi, |

| | | |
|---|---|---|
| | | kulinda mazingira na bainuwai na kuhifadhi mila, desturi na tamaduni<br>• Wakulima na wafugaji washauriwe namna bora ya kufanya kilimo na ufugaji endelevu ili kuendana na mahitaji ya ardhi na rasilimali zake<br>• Sekta ya madini ishauriwe na izingatie matumizi endelevu ya ardhi |
| 10. | Kasi ndogo ya uandaaji wa mipango ya matumizi ya ardhi. Kati ya vijiji takribani 12,545 vilivyopo nchini, ni vijiji 1731 tu (hadi kufikia Mei 2017) vimeandaliwa mipango ya matumizi ya ardhi. | Uandaliwe mkakati wa wa pamoja kati ya Taasisi za Umma na Asasi za Kiraia wa kufikia malengo ya kuandaa mipango ya matumizi ya ardhi ya wilaya 25 na vijiji 7500 kati ya mwaka 2015-2020. |
| 11. | Mipango ya matumizi ya ardhi inaandaliwa lakini haitekelezwi. | • Sheria zinazohusiana na usimamizi wa matumizi ya ardhi lazima zitekelezwe<br>• Ushirikishwaji wa wananchi na jamii kwa ujumla lazima uzingatiwe zaidi ili waelewe na waweze kusimamia na kutekeleza mipango ya matumizi ya ardhi<br>• Wadau waungane pamoja ili kutumia rasilimali walizonazo kutekeleza mipango ya matumizi ya ardhi. |
| 12. | Kukosekana kwa kanzidata (database) ya mipango ya matumizi ya ardhi | Kuanzisha kanzidata (database) itakayoonyesha idadi ya vijiji vyenye mipango ya matumizi ya ardhi, hali halisi iliyofikiwa (status) na njia ya kubadilishana taarifa za mipango ya matumizi ya ardhi baina ya wadau, na asasi za kiraia ili kujua walipo na kazi wanazofanya |
| 13. | Tume kutokuwa na ofisi katika | Tume iwe na wawakilishi katika kanda zote |

| | | |
|---|---|---|
| | kanda zote zitakazokuwa na jukumu la kusimamia mipango ya matumizi ya ardhi | watakaokuwa na jukumu la kusimamia mipango ya matumizi ya ardhi katika kanda hizo. |
| 14. | Mkakati wa uratibu wa uandaaji na usimamizi wa mipango ya matumizi ya ardhi haujulikani kwa wadau | Mkakati wa uratibu wa uandaaji na usimamizi wa mipango ya matumizi ya ardhi ulioboreshwa na wadau ukamilishwe, usambazwe kwa wadau na uwezeshwe utekelezaji wake. |
| 15. | Ushirikiano hafifu na uhaba wa taarifa za mipango ya matumizi ya ardhi baina ya Sekta za Serikali zinazohusika na ardhi, Washiriki wa Maendeleo, Taasisi Binafsi, Taasisi za Elimu ya Juu, na Asasi za Kiraia | Yaandaliwe makubaliano (Memorandum of Understanding) baina ya Sekta za Serikali zinazohusika na ardhi, Washiriki wa Maendeleo, Taasisi Binafsi, Taasisi za Elimu ya Juu, na Asasi za Kiraia kwa ajili ya kufanya kazi pamoja na ubadilishanaji wa taarifa. |
| 16. | Mpango wa Taifa wa Matumizi ya Ardhi (*The National Land Use Framework Plan 2013-2033)* na programu zake hazitekelezwi na hazijulikani kwa wadau | Mpango wa Taifa wa Matumizi ya Ardhi pamoja na programu zake uzinduliwe rasmi ili kuutambulisha kwa wadau kwa ajili ya utekelezaji |

## 5. MKAKATI WA KUTATUA CHANGAMOTO ZA UPANGAJI, UTEKELEZAJI NA USIMAMIZI WA MIPANGO YA MATUMIZI YA ARDHI

Changamoto na mapendekezo yaliyoainishwa na wadau kama ilivyoonyeshwa katika **Jedwali Na. 1** ndio chimbuko la kuandaliwa kwa Mpango kazi wa Kukabiliana na Changamoto za Upangaji, Utekelezaji na Usimamizi wa Mipango ya Matumizi ya Ardhi nchini. Kati ya changamoto zilizobainishwa katika **Jedwali Na. 1** hapo juu, uchambuzi ulifanyika na kupata changamoto kuu 8 kama ifuatavyo;

a) Upangaji wa matumizi ya ardhi kutopewa kipaumbele hivyo kuwepo kwa kasi ndogo ya uandaaji wa mipango ya matumizi ya ardhi nchini,

b) Kukosekana kwa mipango ya matumizi ya ardhi katika ngazi mbalimbali na usimamizi duni wa mipango iliyopo kusababisha kuongezeka kwa migogoro ya ardhi,
c) Upungufu/uhaba wa kanzidata ya wadau na taarifa za mipango ya matumizi ya ardhi,
d) Ushiriki mdogo wa wanawake na makundi mengine katika jamii katika uandaaji, utekelezaji na usimamizi wa mipango ya matumizi ya ardhi,
e) Kutokuwepo na uratibu na mawasiliano ya kutosha baina ya Serikali, Asasi za kiraia na wadau wa maendeleo katika upaagaji, utekelezaji na usimamizi wa mipango ya matumizi bora ya ardhi,
f) Mipango ya matumizi ya ardhi inaandaliwa lakini haitekelezwi na pia baadhi ya vijiji vyenye mipango kugawanywa
g) Programu za Mpango wa Taifa wa Matumizi ya Ardhi wa 2013 -2033 hazitekelezwi na hazijulikani kwa wadau na
h) Ufuatiliaji na tathmini hafifu ya utekelezaji wa mipango ya matumizi ya ardhi.

## 5.1 MPANGO KAZI WA KUPATIA SULUHISHO CHANGAMOTO NA KUTEKELEZA MAPENDEKEZO YALIYOTOLEWA NA WADAU

Baada ya kubainisha changamoto kuu 8 za upangaji, utekelezaji na usimamizi wa mipango ya matumizi ya ardhi nchini, mpango kazi wa utekelezaji wa mapendekezo yaliyotolewa na wadau umeandaliwa kwa kuzingatia changamoto husika, visababishi na mikakati ya utatuzi. Vile vile mpango kazi (**Jedwali Na. 2**) umeainisha mahitaji ya rasilimali fedha pamoja na wadau wanaohusika katika kutekeleza kazi husika. Kazi zilizoainishwa zitatekelezwa katika kipindi cha miaka mitano kuanzia Mwaka wa Fedha 2016/17.

## Jedwali Na. 2: Mpango Kazi wa Kutatua Changamoto na Kutekeleza Mapendekezo ya Wadau Kuhusu Mipango ya Matumizi ya Ardhi Nchini Kuanzia Mwaka 2017 hadi 2021

| Na. | Changamoto | Visababishi | Malengo | Mikakati | Kazi za Kufanyika | Matokeo Tarajiwa | Mahitaji ya Rasilimali (Fedha) | Wahusika wa Kutekeleza | Muda wa Utekelezaji (Miaka) | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | | | | | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 |
| 1. | Kukosekana kwa mfumo jumuishi wa taarifa za mipango ya matumizi ya ardhi | Ukosefu wa fedha | Kuwa na kanzidata jumuishi/unganishi yenye taarifa sahihi za mipango ya matumizi ya ardhi | Kushirikisha wadau mbalimbali kuchangia fedha kwa ajili ya utekelezaji | Kufanya tathmini ya mahitaji ya mfumo jumuishi/unganishi wa kanzidata | Kutambuliwa/kujulikana kwa mahitaji ya mfuno jumuishi/unganishi wa kanzidata | 15,000,000 | NLUPC, Wizara na Taasisi Zinazohusiana na Masuala ya Ardhi, CSOs/NGOs/FBOs/ INGOs/DPs, H/W zote, Sekta Binafsi | ✓ | ✓ | | | |
| | | Kutokuwepo kwa mawasiliano baina ya wadau | | Kuimarisha kituo cha taarifa cha Tume na kuanzisha mfumo unganishi wa kupata taarifa sahihi za mipango ya matumizi ya ardhi | Kununua vifaa vya kwa ajili ya kanzidata | Kuwepo kwa vifaa kwa ajili ya kutunzia na kuendesha mfumo jumuishi wa taarifa za mipango na matumizi ya ardhi | 90,000,000 | NLUPC, Wizara na Taasisi Zinazohusiana na Masuala ya Ardhi, CSOs/NGOs/FBOs/ INGOs/DPs, H/W zote, Sekta Binafsi | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ |
| | | | | | Kuanzisha akaunti za mitandao ya kijamii (blogu, fesibuku na twita) na kuboresha tovuti ya Tume | Wadau kupata kwa urahisi taarifa sahihi za mipango ya matumizi ya ardhi | 8,000,000 | NLUPC, CSOs/ /FBOs/INGOs/DPs | ✓ | ✓ | | | |
| | | | | | Kuanzisha mfumo unganishi wa kanzidata | Kuwepo kwa mfumo unganishi wa kanzidata | 150,000,000 | | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ |
| | | | | | Kutoa elimu kwa wadau juu ya matumizi ya mfumo | Kuongezeka kwa taarifa kutoka na kwenda kwa wadau | 250,000,000 | NLUPC, Wizara na Taasisi Zinazohusiana na Masuala ya Ardhi, CSOs/NGOs/FBOs/ INGOs/DPs,H/W zote,Sekta Binafsi | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ |
| | | | | | | Kuwepo kwa mawasiliano baina ya wadau kupitia mfumo | | | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ |
| | **Jumla Ndogo ya Mahitaji ya Fedha** | | | | | | **513,000,000** | | | | | | |

| Na. | Changamoto | Visababishi | Malengo | Mikakati | Kazi za Kufanyika | Matokeo Tarajiwa | Mahitaji ya Rasilimali (Fedha) | Wahusika wa Kutekeleza | Muda wa Utekelezaji (Miaka) | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | | | | | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 |
| 2. | Upangaji wa matumizi ya ardhi kutopewa kipaumbele hivyo kuwepo kwa kasi ndogo ya uandaaji wa mipango ya matumizi ya ardhi nchini | Viongozi wa Kitaifa kutoipa kipaumbele na umuhimu wa mipango ya matumizi ya ardhi | Upangaji wa matumizi ya ardhi nchini kupewa kipaumbele katika mipango ya kitaifa | Kuhamasisha Viongozi wa kitaifa juu umuhimu wa upangaji wa matumizi ya ardhi | Kuandaa andiko la umuhimu wa upangaji wa matumizi ya ardhi kupewa kipaumbele katika mipango ya kitaifa (BLM) | Upangaji wa matumizi ya ardhi kuwa kipaumbele muhimu katika mipango ya kitaifa | 20,000,000 | NLUPC, Wizara na Taasisi zinazohusiana na maswala ya Ardhi, CSOs/NGOs/FBOs/ INGOs/DPs, H/W zote, Sekta Binafsi | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ |
| | | | | Kuhamasisha viongozi wa Kitaifa na wadau wengine juu ya umuhimu wa mipango ya matumizi ya ardhi | Kuhamasisha Mawaziri na Kamati ya Bunge inayoshughulikia masuala ya ardhi | Mipango ya Serikali na Maazimio ya Vikao vya Bunge kuweka umuhimu wa upangaji wa matumizi ya ardhi | 150,000,000 | NLUPC, Wizara na Taasisi zinazohusiana na maswala ya Ardhi, CSOs/NGOs/FBOs/ INGOs/DPs, H/W zote, Sekta Binafsi | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ |
| | | | | | Kuhamasisha Wakurugenzi Watendaji wa Wilaya, Wakufunzi, Madiwani na Wanavijiji kuhusu upangaji matumizi ya ardhi katika ngazi mbalimbali | Viongozi katika ngazi ya Wilaya na Vijiji kuwa na uelewa na kutenga fedha za upangaji wa matumizi ya ardhi katika maeneo yao | 260,000,000 | NLUPC, Wizara na Taasisi zinazohusiana na maswala ya Ardhi, CSOs/NGOs/FBOs/ INGOs/DPs, H/W zote, Sekta Binafsi | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ |
| | | | | | Kupanga matumizi ya ardhi ya Wilaya 25 | Kuwa na mipango ya matumizi ya ardhi ya Wilaya 25 | 1,675,000,000 | NLUPC, Wizara na Taasisi zinazohusiana na maswala ya Ardhi, CSOs/NGOs/FBOs/ INGOs/DPs, H/W zote, Sekta Binafsi | | | | | |
| | | | | | Kupanga matumizi ya ardhi ya vijiji 7500 | Kuwa na mipango ya matumizi ya ardhi ya vijiji 7500 | 11,775,000,000 | | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ | ✓ |
